MAMLAKA YA HALI YA HEWA
TANZANIA

# JARIDA LA HALI YA HEWA

**Na: 24. Msimu wa Kilimo 2017/18 Tathmini ya Kipindi cha Mei 21-31, 2018 na Matazamio kwa Kipindi cha Juni 01-10, 2018**

**Muhtasari**


- Vipindi vya hali ya ukavu vinatarajiwa kusaidia kukomaa kwa mazao kuelekea uvunaji na uhifadhi katika baadhi ya maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka.
- Athari zitokanazo na uvamizi wa viwavi jeshi zinaweza kuhatarisha usalama wa chakula katika maeneo ya Arumeru na Kilosa.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA MEI 21-31, 2018

Katika kipindi hiki cha siku kumi zilizopita (dekadi) migandamizo mikubwa ya hewa iliyo kaskazini mwa dunia (Azores na Siberia) iliendelea kudhoofika wakati ile iliyopo sehemu ya kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuimarika. Ukanda wa mvua (ITCZ) ulielekea kaskazini zaidi. Joto la bahari katika maeneo ya kusini magharibi mwa bahari ya Hindi lilikuwa la wastani hadi juu kidogo ya wastani na kusababisha uwepo hafifu wa vimbunga baharini, hata hivyo kulikuwa na joto la bahari la juu ya wastani katika eneo la Pwani ya Afrika Mashariki hali iliyopelekea uwepo wa vimbunga kaskazini magharibi mwa Pwani ya Somalia na kusababisha upungufu wa mvua na upepo mkali katika Pwani Tanzania. Upepo ulivuma kutoka kusini hadi kusini mashariki katika maeneo mengi ya nchi. Eneo la Kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) kuliendelea kuwepo na joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani. Hali hii ilisababibisha kupungua kwa mifumo ya kusababisha mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi

## MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA MEI 21-31, 2018

Katika kipindi cha siku kumi zilizopita, mvua za masika zimeendelea katika baadhi ya maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua hususani maeneo ya nyanda za juu kaskazini pamoja na kanda ya ziwa Victoria. Hata hivyo baadhi ya maeneo ya pwani ya kaskazini yalipata mvua chini ya mm 10 kielelezo.



**Kielelezo Na. 1**. Kiasi cha mvua kipindi cha tarehe 21-31, May, 2018.

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA MEI 21-31, 2018

Katika kipindi cha dekadi iliyopita, baadhi ya maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua wakulima waliendelea na shughuli za uvunaji wa mahindi wakati kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua mahindi yapo katika hatua ya kubeba. Hata hivyo, mikoa ya Iringa, Mbeya, Njombe and Singida mahindi yapo katika hatua ya kubeba na kukomaa. Maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka, hususan mikoa ya Tanga, Pwani, Mara, Kagera na Morogoro magharibi, mahindi yameanza kukomaa.

Maharagwe yana hali nzuri na yapo katika hatua ya kukomaa katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua. Mpunga pia unaendelea kuvunwa maeneo ya Kigoma, Mwanza, Shinyanga, Rukwa na Tabora. Mikoa ya Mwanza, Kigoma na Shinyanga wakulima wanaendelea na shughuli za uvunaji wa pamba. Imetaarifiwa kuwepo kwa athari kubwa za Viwavi jeshi katika mikoa ya Morogoro (wilaya ya Kilosa) na Arusha (wilaya ya arumeru). Hali ya maji na malisho kwa ajili ya wanyama ilikuwa ya kuridhisha.

## HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA MEI 21-31, 2018

Kina cha maji katika mabwawa, mabonde na mtiririko wa maji katika mito ilikuwa ya wastani

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 01-10, 2018

Katika kipindi hiki, Migandamizo mikubwa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kudhoofika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kuimarika. Ukanda wa mvua (ITCZ) unatarajiwa kuendelea kusogea kuelekea kaskazini hali itakayopelekea upepo kuvuma kutoka kusini hadi kusini mashariki katika maeneo mengi ya nchi. Joto la bahari la wastani linatarajiwa katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi hali itakayopunguza uwezekano wa kutokea vimbunga katika bahari. Upepo unatarajiwa kuvuma kutoka kusini hadi kusini mashariki hali itakayopekekea hali ya baridi katika baadhi ya maeneo hasa yale yaliyoko kusini mwa nchi. Eneo la Kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) kunatarajiwa kuwa na joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani. Hali hii itapelekea kupunguza kwa upepo uvumao kutoka magharibi hivyo kupunguza nguvu ya mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi.

## HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MEI 01-10,2018

Katika kipindi cha siku kumi zilizopita Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) inatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua vitakavyo ambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache hususan katika siku tano za mwanzo.

Nyanda za juukaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) inatarajiwa kuwa na mvua nyepesi katika maeneo machache hususani katika maeneo ya miinuko. Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwavya Unguja na Pemba) na Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi) inatarajiwa kuwa na mvua nyepesi katika maeneo machache. Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora), Nyanda za juu Kusinimagharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) na Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa Morogoro) inatarajiwa kuwa na mawingu kiasi kwa ujumla. Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida) inatarajiwa kuwa na mawingu kiasi

## MATARAJIO NA USHAURI WA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA JUNI 1-10, 2018

Katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua, hali ya ukavu inayotarajiwa itasaidia uvunaji, ukaushaji na uvunaji wa mazao. Athari zitokanazo na shambulio la Viwavijeshi kwa wilaya za Arumeru na Kilosa zinatarajiwa kuathiri usalama wa chakula katika maeneo hayo, hivyo wakulima wanashauriwa kuweka akiba ya ziada ya chakula kuepuka janga la njaa. Hali ya maji pamoja na malisho vinatarajiwa kuimaraika katika maeneo mengi ya nchi.Wakulima, wavuvi na wafugaji wanashauriwa kuwasiliana na maofisa ugani kwa ajili ya kupata ushauri na matumizi sahihi ya utabiri huu.

## HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 01-10,2018

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kupungua katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua. Wananchi wanashauriwa kutumia maji kwa uangalifu.

*Jarida limetayarishwa na:*

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

***S.L.P 3056; Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 ; Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz***